# Hadithi 1

## VIPAUMBELE VYA DINI

Kutoka Ibn Abbas (r.a) amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu rehma na amani ziwe juu yake, kumwambia Mua'dh ibn Jabal wakati alipomtuma kwenda yemen:

1 "Hakika wewe utawaendea watu wa kitabu

2 Utakapo waendea, walinganie kwenye shahada wakiri kwa moyo kuwa hakuna mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa yeye peke yake, na hakika Nabii Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu.

3 Ikiwa watakukubalia hilo, basi waeleze kwamba hakika Mwenyezi Mungu amewafaradhishia sala tano mchana na usiku.

4 Ikiwa watakukubalia hilo, basi waeleze kuwa Mwenyezi Mungu amewafaradhishia juu yao, zaka ya mali zao, inachukuliwa kutoka kwa matajiri wao na inapelekwa kwa maskini wao.

5 Ikiwa watakukubalia hilo, basi jiepushe na kuchukua malizao bora zaidi.

6 Na ogopa dua ya aliye dhulumiwa, kwani hakika hakuna kati yake na Mwenyezi Mungu pazia" . Imepokelewa na Bukhari na Muslimu.[1]

1 Sahihi Al-Bukhari (1496), na Sahihi Muslim (19).

### Ayah

*Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:*

*﴿Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia ya kwamba hapana mungu isipo kuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu. (25)﴾ [Al-Anbiyaa].*

*﴿Amesema Allah mtukufu. Shika Sala jua linapo pinduka mpaka giza la usiku, na Qur'ani ya al fajiri. Hakika Qur'ani ya alfajiri inashuhudiwa daima. Al-Israa. Amesema Allah mtukufu﴾*

*﴿Chukua sadaka katika mali zao, uwasafishe na uwatakase kwazo, na uwaombee rehema. Hakika maombi yako ni utulivu kwao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mwenye kujua. (103) Je! Hawajui ya kwamba Mwenyezi Mungu anapokea toba ya waja wake, na anazikubali sadaka, na kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kupokea toba na Mwenye kurehemu.(104) At-Tawba Amesema Allah mtukufu)﴾*

*﴿Wa kupewa sadaka ni mafakiri, na masikini, na wanao zitumikia, na wa kutiwa nguvu nyoyo zao, na katika kukomboa watumwa, na wenye madeni, na katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na wasafiri. Huu ni waajibu ulio faridhiwa na Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua Mwenye hikima. (60)﴾ [At-Tawba].*

*﴿Amesema Allah mtukufu. Au nani yule anaye mjibu mwenye shida pale anapo mwomba, na akaiondoa dhiki, na akakufanyeni warithi wa ardhi? Je! Yupo mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Ni machache mnayo yazingatia. (62)﴾ [An-Naml].*

### Msimulizi

jina lake anaitwa: Abu al-Abbas, Abdullah bin Abbas bin Abdul Muttalib, al-Qurashi, al-Hashemi, al-Madani, alizaliwa katika watu wa Bani Hashim miaka mitatu kabla ya kuhama, na yeye ni mwanzuoni nguri katika ummah huu, na mtafsiri hodari wa Qur'an, binamu wa Mtume wa Allah, rehma na Amani zimshukie, na alikuwa akiitwa: bahari, kwa sababu ya elimu yake kubwa, Mtume (rehema na amani za Allaah ziwe juu yake) alikumombea dua kwa kusema: "Ewe Allah, mfahamishe elimu ya dini[1]", na yeye ni mmoja wa maswahaba walisimulia hadithi nyingi, alisemulia hadithi (1696) kutoka kwa Mtume (rehema na amani za Allaah zimshukie) aliingia katika uislamu akiwa kijana mdogo, na akalazimiana na Mtume (rehema na amani za Allaah zimshukie) baada ya vita ya ufunguzi wa makkah, na alipokufuka macho mwishoni mwa maisha yake, na alifariki katika mji wa Taif mwaka (68 AH)[2].

### Muhtasari

Mtume (rehema na amani za Allaah zimshukie) alituma Muaadhi kwenda Yemen, na akamueleza namna ya kulingania watu, kwanza alimuhusia kulingania katika kumpwekesha Allah, na kama walitii hilo na kukubali kuwa Waislamu, basi awaeleze uwajibu wa swala tano, na kisha awajulishe ulazima wa zaka.

Kisha akamwagiza Mu'adh aepuke mali zao pendwa , asizichukue kama zaka au sadaka, bali achukue zili za katika na katika, sio zilizo bora wala mbaya zaidi. Pia alimwonya juu kudhulumu haki, kwani dua ya mwenyekudhulumiwa

1 Imesimuliwa na al-Bukhaari (143) na Muslim (2477).

2 Angalia tafsiri yake katika: Maarifa as-Sahaba na Abu Na'im (3/1699), al-Ta'sab fi 'Arif al-Sahib na Ibn 'Abd al-Barr (3/933), Asad al-Ghabah na Ibn al-Atheer (3/291).

# Ufahamu

Alimtuma Mtume (s.a.w) Mua'dh kwenda yemen hali akilingania na akisimamia hukumu, karibia kabisa na mwaka wa tisa hijiriya(9h):

1 Na akamweleza kwamba atawaendea watu katika mayahudi au manaswaara miongoni mwa waliokua na kitabu cha taurati au injili, ili ajiandae kwakuwa wao walikuwa ni watu wenye elimu kiujumla[1].

2 Kisha akamuusia aanze kuwalingania juu ya kukiri upweke wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kuukubali utume wa nabii wake (s.a.w), kwa sababu kuyakubali hayo mawili ndio msingi wa dini ambao hakitakubalika chochote katika matawi yake ila baada ya kuikubali misingi hiyo miwili, hivyo basi inawapasa kuelewa misingi hiyo,[2] kwani mayahudi na manaswara hawakutekeleza yale ambayo ingekuwa ni sababu ya kuwaokoa, kama kushuhudia kwa kukubali kumpwekesha Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kuukubali utume wa nabii Muhammad(s.a.w), basi wao walimshirikisha Mwenyezi Mungu pamoja na Issa ibn Maryam, na wakakanusha da'wah ya Mtume (s.a.w)[3].

3 Kisha akamweleza Mtume (s.a.w) kwamba wakifuata utakayo waamrisha kwa kutamka shahada mbili, na wakakubali kumpwekesha Mwenyezi Mungu na wakakubali utume wa Nabii Muhammad (s.a.w), basi wajulishe kwamba hakika Mwenyezi Mungu amewafaradhishia kusali sala tano mchana na usiku, na uwafundishe namna ya kusali.

Na hakika yamejulisha maneno ya Mtume (s.a.w): "Ikiwa watakukubalia hilo" juu ya kufuata kiutendaji sio alimradi kukubali uwajibu na ulazima, hivyo basi ni lazima wakubali na watekeleze sala katika nyakati zake[4].

4 Kisha akaenda hatua kwa hatua baada ya kukubali uwajibu wa sala na kuitekeleza kwake, akahamia kwenye zaka, akamuamrisha awafundishe kwamba Mwenyezi Mungu amewalazimisha matajiri kutoa zaka, nacho ni kiwango kidogo kinachojulikana kinakusanywa kutoka katika mali zao, na kinagawiwa kwa masikini wao.

---

1 Fath al-Bari cha Ibn Hajar (3/358).

2 "Kashfu Litham ufafanuzi wa Umdat al-Ahkam" cha al-Saffarini (3/400).

3 Kumkamilisha Mwalimu kwa Faida za Muislamu cha Qaadh Iyadh (1/239).

4 Tazama: "katika ufafanuzi wa al-'Umdah cha Ibn al-Attar" (2/798).

5 Kisha akamuamrisha Mtume (s.a.w) Mua'dh (r.a) ikiwa watu watamkubalia hilo na wakatoa zaka ya mali zao, basi achukue kiasi maalum cha zake na ajiepushe na kutoa mali nzuri ambazo wanazipenda wenye mali hizo na nafsi zao zimefungamana na mali hizo kwa kuzipenda; kama mfano, mtu akiwa na mbuzi anaempenda zaidi na anampatia kipaumbele zaidi ima kwa wingi wa maziwa yake, au kwa sababu nyingine, basi mfano wa mbuzi huyo hatakiwi kuchukuliwa katika zaka, kwa kuwafanyia upole wenye mali, na Mwenyezi Mungu hakujaalia kuwaliwaza masikini katika kuwapitasha madhara matajiri, na ikiwa nafsi ya tajiri ikiridhika kwa kutoa kitu bora zaidi, basi itafaa kuchukua kwa ridhaa yake. Na amesema Omar ibn Al-khatwab (r.a) kumwambia mtu aliye mtuma kukusanya zaka: "Na usichukue katika zaka mnyama bora alienenepeshwa ili achinjwe, wala ruba- ambaye huwa anabakishwa nyumbani wala haachwi kujitafutia chakula kutokana na uzuri na ubora wake kwa anaemmiliki, wala mwenye mimba- ambaye anakaribia kuzaa, wala dume tegemezi katika wanyama"[1].

6 Kisha akamtahadharisha Mtume (s.a.w) na mwisho mbaya wa kudhulumu, katika kukusanya zaka au katika mambo mengine ya kiutawala na kihukumu, na kujiweka mbali na dua ya mwenye kudhulumiwa: ni kujiepusha na sababu zake; kwa sababu dhulma- ndio inapelekea kupatikana maombi mabaya dhidi ya mwenye kudhulumu.

Na ya mwenye kudhulumiwa huwa inasikika zadi na kujibiwa na wala hairudi patupu, hufunguliwa milango saba ya mbingu, na hakuna kizuizi kati yake na kujibiwa kwake[2], katika hadithi: " Watu watatu duwa zao hazirudi patupu-bila majibu-: mwenye kufunga saumu mpaka afungue, na kiongozi mwadilifu, na maombi ya mwenye kudhulumiwa, anayanyanyua Mwenyezi Mungu maombi hayo mawinguni na anayafungulia milango ya mbingu na anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: " Naapa kwa nguvu zangu nitakunusuru hata baada ya muda"[3].

---

1 Malik (2/372), na al-Tabarani katika Kamusi Kuu (6395). Na ameisahihisha Al-Nawawi katika "Al-Majmuu'" (5/427), na Ibn Katheer kaboresha upokezi wake katika "Irshad Al-Faqih" (1/248).

2 Fath Al-Mun'im ufafanuzi wa Sahih Muslim cha Musa Shaheen Lashin (1/70).

3 Al-Tirmidhiy (3598), na Ibn Majah (1752), kutoka kwa Abu Hurayrah, na meisahihisha Ibn al-Mulqin katika "Al-Badr al-Munir" (5/152).

# Mafunzo

1. Nabii Muhammad (s.a.w) alimtuma Mua'dh ibn jabal kwenda yemen akiwa kwenye miaka ya ishirini katika umri wake, basi akavumilia mazingira ya ugeni na kuwa mbali na watu wake katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kutii amri ya Mtume (s.a.w), ni mara ngapi sisi tunavumilia matatizo na majukumu kwa ajili ya njia hiyo?

2. Alikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu rehma na amani ziwe juu yake, akiwabebesha maswahaba zake majukumu mazito na makubwa, hali wakiwa katika ujana wao, na wao hawakuwa wakiyakimbia majukumu hayo, hivyo basi ni juu ya baba, mzazi, mwalimu, mlezi na wengineo kuwaandaa na kuwazoesha walioko chini yao kuwapa majukumu, na wasiwadogeshe, na ni juu ya hao pia kuyapokea vyema majukumu hayo na kuyafanyia kazi.



3. Chukuwa yaliyo sihi miongoni mwa maneno ya Mtume Muhammad (s.a.w), japo akiwa mpokezi au msimulizi wake ni mmoja, kwani alimtuma Mtume (s.a.w) Mua'dh akiwa peke yake kwa mambo makubwa miongoni mwa itikadi na ufahamu, na kutoka katika mamlaka hata katika mali za watu, na yote hayo yanajulisha juu ya kuzingatia maneno ya mtu mmoja.

4. Jifunze kujua tabia za unao waendea, hakika alimueleza Mtume (s.a.w) Mua'dh (r.a) ya kwamba atawaendea watu waliopewa kitabu, ili kuchunga yanayo paswa kuwalingania[1], katika vipaumbele vya dalili na njia za kulingania na mambo mengine, kwa sababu wao ni watu wa elimu na mijadala, basi pupia kukusanya taaluma ya kutosha na yenye athari, kabla ya kazi yoyote unayotaka kuifanya.

5. Mtume (s.a.w) alitilia umuhimu zaidi kuwaelekeza wafanyakazi wake na watoa mawaidha, kwakuwa yeye hakumtuma Mua'dh mpaka alipombainishia hali halisi, na pia akampangia kazi, na akamuamrisha kuwa mwadilifu, na akamtahadharisha kutokana na kudhulumu, pamoja na ukamilifu wa Mua'dh kwenye dini yake na elimu yake, basi usiache kumuusia uliye naye, na inampasa anaye pewa wosia kutopuuza wosia huo.

1 Fath al-Bari cha Ibn Hajar (3/358).

6 Mtume (s.a.w) alitilia umuhimu zaidi vipaumbele vya kwanza kisha akaenda hatua kwa hatua, ndio maana hakumuamrisha Mua'dh kuanza na madhambi ambayo watu hawaepukani nayo katika maisha yao na tabia zao, pamoja na kuwepo umuhimu wa kuyakemea hayo, lakini alianza na misingi ya dini, na funguo za imani nao ni shahada mbili, kisha sala, kisha zaka, na hivi ndio tunatakiwa kuwa katika malezi yetu na ulinganiaji wetu na kusomesha kwetu, bali tunapaswa kufanya hivyo katika kazi zetu zote, tuanze na lililo muhimu zaidi kisha linalo fuatia kwa umuhimu, amesema A'ishat (r.a) "Si vinginevyo hakika ufunuo wa kwanza ulioteremka katika ufunuo ni sura zilizo pambanuliwa, katika hizo pametajwa pepo na moto, mpaka watu walipoufuta uislamu ikateremka katika ufunuo yaliyo halali na haramu, kama ingeteremka mwanzoni tu " msinywe pombe" basi watu wangesema hatutaacha pombe milele, na kama ingeteremka mwanzoni "msizini" basi wangesema hatuwezi acha zinaa milele"[1].

7 Imani, sala na zaka, ndio misingi ya imani kubwa ambayo imekaririwa kwa kukutanishwa katika qur'ani tukufu na maneno ya Mtume (s.a.w) kwa wingi sana, na ndani yake kuna malipo makubwa (thawabu) na kuathirika kiimani, kwa kiasi ambacho hakuna akijuaye isipokuwa ni Mwenyezi Mungu Mtukufu, basi hata ukiwa wewe na wenzako mnatekeleza misingi hiyo basi pupieni kuifanya kikamilifu.

8 Alimtahadharisha Mtume Muhammad (s.a.w) Mua'dh kuchukua zaka ambayo nafsi zimefungamana nazo kutokana na ubora na uzuri wa sadaka hiyo, bali alimuamuru kuwa mwadilifu, na kufanya hivyo ni katika uadilifu na kuchunga hisia za watu na uelewa wa watu ambao ni juu ya kila mlinganiaji na baba na mlezi mwenye kusimamia mambo afanye kama hivyo, basi azingatie hayo katika kuamrisha kwake na kukataza kwake.

9 pupia kulala hali yakuwa hakuna aliye dhulumiwa ambaye kakosa kulala kutokana na huzuni kwa yale uliyoyasema au kumtendea,sawasawa awe ni mume au mtoto, au mwanafunzi au mfanyakazi, au mfanya biashara au dereva, na wala usiirahisishe dhulma kwa yule unaye muona yuko chini yako, japo akiwa katika waasi, na hakika alimuhofisha nabii muhammad (s.a.w) Mua'dh kutokana na dhulma upeo wa kuhofisha,hata katika kutaamali na makafiri miongoni mwa watu wa kitabu, na baadhi yao wanaweza kuamini na wengine wasiamini.

**Amesema mshairi:**

Usifanye dhulma katu hata ukiwa na uwezo wa kufanya hivyo = kwani hakika dhulma mwisho wake inakuletea majuto

Macho yako yanasinzia huku aliyedhulumiwa halali yuko macho = akikuombea dua mbaya na jicho la Mwenyezi Mungu halilali.

1 Sahihi Al-Bukhari (4993).

